

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**  
**MUHTSARI WA KIKAO CHA DCC KILICHOFANYIKA TAREHE 06/02/2017**  
**KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA**

**WALIOHUDHURIA**

- |   |                                       |
|---|---------------------------------------|
| 1. MH. LT. COL. MICHAEL MNTENJELE             | MWENYEKITI (DC)                       |
| 2. BW. AIDAN J. BAHAMA                        | KATIBU (DED)                          |
| 3. BW. VEDASTUS TIBAIJUKA                     | DAS                                   |
| 4. MH. ERICK E. NKILAMACHUMU                  | M/KITI WA HW (DIWANI)                 |
| 5. MH. WILBARD BAMBARA                        | M/M/KITI WA HW(DIWANI)                |
| 6. BW. KAPAMA FELICIAN                        | MKAGUZI WA NDANI(W)                   |
| 7. BW. MKUBWA G.I                             | MCHUMI                                |
| 8. MH. KAGOMBAGEORGE                          | DIWANI-MUGOMA                         |
| 9. BW.SUBIRA MANYAMA<br>UJENZI(W)             | K/MHANDISI WA                         |
| 10. BW. DAVID BUKOZO                          | KATIBU-MAT                            |
| 11. BW. DEUSDENT KATO                         | K/ MRATIBU WA TASAF(W)                |
| 12. BI. PALITHA CLEOPHAS<br>MSINGI(W)         | K/ AFISA ELIMU                        |
| 13. BW. DAVID BUKOZO                          | MAT                                   |
| 14. MH. JOHN SHIM'IMANA                       | DIWANI-KIBIMBA                        |
| 15. MH. GWIHANGWE M. EDWARD                   | DIWANI-NGR-MJINI                      |
| 16. MH. GWASSA NTUNGIYE                       | DIWANI-NYAMIAGA                       |
| 17. BW. SYPRIAN BIHERERE                      | K/ AFISA TARAFKA-KANAZI               |
| 18. BW. JOHN SOSTHENES                        | K/ AFISA KILIMO(W)                    |
| 19. BW. GASPAR KAPARAGA                       | AFISA KILIMO                          |
| 20. BW. HERMAN HUME<br>JAMII(W)               | AFISA MAENDELEO YA                    |
| 21. BW. RUKIZA ABEID                          | AFISA TEHAMA                          |
| 22. BI. GWANBASA G.J                          | Ag. DWE                               |
| 23. BW. SELIALIS ANTONY                       | TEO-RULENGE                           |
| 24. BW. SIMEON NDYAMUKAMA                     | MHANDISI WA MAJI                      |
| 25. BW. MOSES KICHOGO                         | AFISA HABARI                          |
| 26. BW. SANGATATI JOSEPHAT                    | AFISA MIFUGO(W)                       |
| 27. BW. TOBA A. MHINA                         | TEO-NGARA MJINI                       |
| 28. MH: MKUBILA SOUD                          | DIWANI-M/SAGAMBA                      |
| 29. MH. KHAMIS HAMAD B.<br>MH: EDITHA MWINULA | DIWANI-RULENGE<br>DIWANI-VITI MAALUMU |
| 30. MH: JUSTUS K. MASUMO                      | DIWANI-NYAKISASA                      |

31. MH: ROMAN M. MITABARO	DIWANI- KEZA
32. MH: NZEYE LEONARD	DIWANI-MUGANZA
33. MH: OLIPA A. BUGOKE	DIWANI VITI MAALUMU
34. MH: SENTORE MIBURO	DIWANI-KIRUSHYA
35. MH: VAILETH MADENDE	DIWANI VITI MAALUMU
36. MH: SUZANA B. NJOJOLI	DIWANI- VITI MAALUMU
37. BW. JULIUS ERENEST NYAMIAGA	K/AFISA                TARAFI-
38. BW. CHRISTOPHER NZOYA	WEO-MUGOMA
39. BW. MORIS MOMBIA RULENGE	K/AFISA                TARAFI-
40. BW. MARWA NYANSWI	DIO
41. BW. ALFRED KAFUKU KATENGA	A/ELIMU SEKONDARI(W)
42. REV. EMMANUEL BISHAZA	PEFA
43. BW. KENEDY. FESTO	M/MKITI CDM(W)
44. BW. FESTO MASHAURI	ASKOFU TAG-NGARA
45. BW. MARTIN LEONARD	TCCIA
46. BW. PETER KAPALALA	WEO-KASULO
47. BW. HURBERT R. NDUNGURU	WEO-MURUKULAZO
48. BW. FADHILI RUSAGE	KATIBU/MBUNGE
49. REV. SIMON RUMITO	PAG BISHOP
50. BW. BENETH RUSULE	WEO-KIBOGORA
51. BW. PASTORY M. MSABILA M/SAGAMBA	AFISA                TARAFI-
52. BI. JASMINI PETER	AFISA UTUMISHI
53. BI. SARAH BANZI	NMB-NGARA
54. BW. MOHAMED RUNZENZA	WEO
55. BW. PHILIMON MPANJU	WEO-NGARA
56. BW. ERENEST CHACHA	MENEJA-CRDB
57. BI. CHRISTINA NGONYANI	WEO-RUSUMO
58. BI. SOPHIA MAPUNDA	WEO-NTOBEYE
59. SH. ABDALLAH ZAKARIA	BAKWATA
60. REV. AMON NZIKUBANKUNDA	AGLICAN
61. SGT MATHIAS PAUL	MMM(W)
62. MH: LAURENT MSUNGARERE	DIWANI-NYAMAGOMA
63. BW. FREDRICK KAKURU	AFISA UCHAGUZI
64. MH: ZAWADI COSMAS	DIWANI VITI MAALUMU
65. BI. JULIETH MUSSA	UNHCR
66. BI. BETTY S. MUNUO MALIASILI(W)	AFISA                ARDHI                NA

67. BW. SLYVESTER MAKUMBA	WEO
68. BW. ERICK ELIAZARY	WEO
69. SISTA FRANSISKA BAZI	NAZARETI CENTRE
70. MH. SAFARI M. BANIGWA	DIWANI-MABAWAWE
71. MH. SAID R.SOUD	DIWANI-KABANGA
72. MH. JOHN E. RUZIGE	DIWANI-NTOBEYE
73. BI. BETTY S. MUNUO	A/ARDHINA MALIASILI(W)
74. BW. BIGAMBO AMOS	AFISA MIPANGO(W)
75. BW. REVOCATUS NDYEKOBORA	DMO(W)
76. BW.MUZORA E. BITESIGIRWE	Ag. DHRO(W)
77. BW. MASOUD B.A	DT(W)
78. MH. REHEMA S. RAMADHANI	DIWANI-VITI MAALUMU
79. MH. GEORGIA MNYONYERA	DIWANI-VITI MAALUMU
80. BW. LAURENT GERVAS	MWANDISHI WA HABARI
81. MH. ADRONIZI BURINDOLI	DIWANI-KIBOGORA
82. MH: MUGATA M.E	DIWANI-KANAZI
83. BW. MOHAMED NGERAGEZA	KATIBU CUF
84. BW. KAMAIZA JULIUS	RADIO- KWIZERA
85. BI. REINFRIDA ANZIGARY	CC (H/W)

### **MUHT NA 1/2017/2018: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alianza kwa kuwasalimia wajumbe na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwezesha kufanikisha kikao cha DCC cha kujadili bajeti 2017/18 kuweza kufanyika, na kumkaribisha Mwenyekiti wa Halmashauri aweze kuongea machache kabla ya kumkaribisha Mwenyekiti(Mh. Mkuu wa Wilaya) aweze kufungua kikao.

Mwenyekiti wa Halmashauri alianza kwa kuwasalimia wajumbe na kuwaomba wajumbe kuweza kujadili bajeti ya mwaka 2017/18 kwa kina kwa ajili ya maendeleo ya Wilaya ya Ngara, aidha alimuomba Mkurugenzi Mtendaji kufanya mwaliko wa wananchi katika kikao cha Baraza la Madiwani kujadili bajeti ili waweze kusikiliza bajeti ya mwaka 2017/18 na kumkaribisha Katibu Tawala aweze kumkaribisha Mwenyekiti aweze kufungua kikao.

Katibu Tawala alimkaribisha Mwenyekiti aweze kufungua kikao. Mwenyekiti alianza kwa kuwasalimia wajumbe na kuwakaribisha, aliwakumbusha Waheshimiwa Madiwani kuwa wana jukumu la kuwaunganisha wanachi na Serikali. Kikao kilifunguliwa saa 4.50 asubuhi.

### **MUHT NA 2/2017/2018: KURIDHIA AGENDA**

Mwenyekiti wa Halmashauri aliwaomba wajumbe kuongeza agenda ya kuwepo kwa majimbo 2 ya uchaguzi katika Wilaya ya Ngara yaani Ngara kusini na Mgara Kaskazini.

Mjumbe mmoja alishauri kwamba kutokana na umuhimu wa jambo hilo ingekuwa vizuri suala hilo likajadiliwa katika kikao.

Mwenyekiti alishauri kwamba agenda hiyo ni muhimu kujadiliwa lakini wananchi wajumbe wangezingatia zaidi umuhimu wa kikao cha agenda mahususi ni ya kujadili bajeti ya mwaka 2017/18. Hivyo agenda hiyo ijadiliwe kikao kijacho.

Katibu aliwaomba wajumbe kumkumbusha ili kikao kijacho agenda hiyo iweze kujadiliwa.

Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliridhia kujadili agenda ya mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2017/18 na agenda ya kuwepo kwa majimbo 2 ya uchaguzi katika Wilaya ya Ngara kujadiliwa katika kikao kijacho.

### **MUHT NA 3/2017/2018: MAPENDEKEZO YA MPANGO WA BAJETI YA MWAKA 2017/18**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa kama ifuatavyo;

Rasimu ya Mpango na Bajeti ya Wilaya ya Ngara kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 umezingatia mambo mbalimbali ya kisera yakiwemo,

- Utekelezaji wa Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2015
- Mpango wa II wa miaka mitano wa Taifa 2016/17 – 2020/21
- Mwongozo wa Bajeti 2017/18
- Vipaumbele vilivyotolewa na Mhe. John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuzindua Bunge la kumi na moja (11) tarehe 20/11/2015.
- Mpango mkakati wa Halmashauri
- Vipaumbele vya Wilaya.

### **1.0 MAENEO YALIYOPEWA KIPAUMBELE KWENYE MPANGO NA BAJETI 2017/18.**

Halmashauri katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo, imeweka vipaumbele vifuatavyo;

- Kuimarisha mapato ya Halmashauri kwa kujenga uwezo wa Tehama na matumizi ya Tehama.
- Kukamilisha Miradi viporo ikiwa ni pamoja na ahadi ya Mhe. Rais Mstaafu Jakaya Mrisho Kikwete.
- Kuimarisha huduma za Afya Kinga, hasa ujenzi wa vyoo Shuleni na usafi wa mazingira.
- Kuimarisha huduma za Afya Tiba hasa upanuzi wa Hospitali (W) na Kituo cha afya Murusagamba na Bukiriro.
- Kuimarisha Maendeleo ya Viwanda kwa kuandaa mpango wa matumizi bora ya Ardhi.
- Kuimarisha Kilimo cha kibiashara hasa kinachoinua uchumi wa Wananchi.

### **3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2015/16.**

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara katika Mwaka wa fedha 2015/16, Serikali Kuu iliidhinisha jumla ya Tshs. 28,060,208,855/= kama ruzuku kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Kati ya hizo Tshs. 19,754,132,000/= kwa ajili ya Mishahara (PE), Tshs. 2,465,420,000/= kwaajili ya matumizi mengineyo (OC), Tshs. 1,682,110,000/= Mapato ya vyanzo vya ndani na Tshs. 4,158,546,855/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia Mwezi Juni, 2016 Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilikuwa imepokea Jumla ya Tshs. 27,339,003,261.17 (97.43%) ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mgawanyo ufuatao; Tshs. 20,352,917,248.93 kwa ajili ya Mishahara, Tshs. 1,853,315,919.60 Ruzuku ya matumizi mengineyo (OC), Tshs. 1,433,433,583.34 Mapato ya vyanzo vya ndani na Tshs. 3,699,326,509.30 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### **4.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2016/17.**

Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya Tshs. 36,018,922,560/= kwa mchanganuo ufuatao; Ruzuku ya Mishahara (PE) Tshs. 25,310,868,000/=, Ruzuku ya Matumizi Mengineyo Tshs. 2,309,303,000/=, Makusanyo ya ndani Tshs. 2,469,016,800/=, Miradi ya Maendeleo Tshs. 5,988,869,360/=.

Hadi kufikia Mwezi Desemba 2016, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilikuwa imekusanya jumla ya Tshs. 16,201,055,161.46/= (45.23%), mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo; Tshs. 12,140,602,855.2 ikiwa ni Ruzuku ya mishahara, Tshs. 559,769,252/= ikiwa ni Ruzuku ya Matumizi mengineyo, Tshs. 710,938,721/= ni mapato ya vyanzo vya ndani na Tshs. 2,708,963,028.22/= ni Ruzuku ya Miradi ya Maendeleo.

Utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri zinaendelea kwa viwango tofauti kutokana na mapokezi ya fedha toka Hazina ikiwa ni pamoja na uratibu wa Mitihani ya darasa la nne, darasa la saba, kidato cha pili na kidato cha nne. Hata hivyo fedha za walengwa wa kaya maskini (TASAF) zinafika kwa wakati wake. Changamoto kubwa ya utekelezaji wa Miradi inatokana na mapokezi ya fedha kutofika kwa wakati na kusababisha Miradi kutokamlika kwa wakati.

#### **5.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA 2017/2018.**

Halmashauri ya wilaya ya Ngara kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 inapendekeza kukusanya na kutumia jumla ya Tshs. **42,810,487,993/=** kwa mchanganuo ufuatao:-

• Ruzuku ya Mishahara	Tshs.	29,959,991,200/=
• Mapato ya Ndani	Tshs.	2,469,016,800/=
• Matumizi mengineyo	Tshs.	2,438,879,184/=
• Miradi ya Maendeleo	Tshs.	7,942,600,809/=
<b>JUMLA KUU</b>	<b>Tshs</b>	<b>42,810,487,993/=</b>

#### **6.0 MAJADILIANO**

Maombi ya fedha kwa Mwaka 2017/2018

Katika Mpango na Bajeti ya mwaka 2017/2018 Halmashauri ya wilaya ya Ngara inaomba kuidhinishiwa jumla ya Tshs. **42,810,487,993/=** (Bilioni arobaini na mbili mia nane na kumi milioni mia nne themanini n asaba elfu n amia tisa tisini na tatu). Kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Mishahara na uendeshaji wa Halmashauri.

Mwenyekiti wa Halmashauri aliwashauri wajumbe kupitia bajeti kwa umakini mkubwa yaani ukurasa kwa ukurasa ili kuweza kuchangia bajeti iliyowasilishwa.

Mwenyekiti alisema kwamba kwenye bajeti iliyowasilishwa Idara ya maliasili namba ya vifungu inajirudia rudia, aliwashauri Wataalamu kuweka vifungu vyote kwenye sehemu moja, Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo- Ngara alijibu kwamba taarifa hutolewa kwenye mfumo moja kwa moja hivyo kwa kutumia mfumo huwezi kuandika vifungu vinavyofanana.

Mwenyekiti wa Halmashauri alihoji ni kwa nini Mamlaka ya Mji Mdogo-Rulenge haijawekwa kwenye bajeti, aidha alieleza kwamba kwenye Baraza la Madiwani la bajeti hatoitisha bajeti endapo bajeti ya Mamlaka ya Mji Mdogo- Rulenge haitowekwa katika mpango wa bajeti, Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo-Ngara alijibu kwamba bajeti ya Mamlaka ya Mji Mdogo- Rulenge imewekwa katika bajeti ya Idara ya Utawala na kama bajeti hizo mbili zingewekwa kwenye mfumo kwa pamoja mfumo usingekubali kuingiza bajeti hizo.

Mwenyekiti alishauri kwamba kwenye gharama za mazishi ziunganishwe na ziwekwe sehemu moja, Afisa Mipango alieleza kwamba mfumo hauwezi kukubali hivyo ilipelekea kila Idara kuweka gharama za mazishi katika kifungu kinachojitegemea.

Mjumbe mmoja alihoji kigezo kilichotumiwa na Halmashauri ya Wilaya kupitisha bajeti ya ushuru wa vibanda kilipwa Tshs. 10,000/= bila kuangalia hali halisi ya kipato na ushuru huo kuwekwa katika maeneo kama Kabanga, Rulenge na Rusumo ambapo makusanyo katika maeneo hayo ni makubwa ukilinganisha na eneo la Ngara Mjini.

Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji-Mdogo Ngara alijibu kwamba vibanda vya Ngara mjini vinatozwa Tshjs. 10,000/= kulingana na sheria ndogo ya Mamlaka iliyotungwa mwaka 2013.

Mjumbe mwingine alitaka kupata ufafanuzi wa kodi ya vibanda inayotozwa na Halmashauri, je kodi hiyo ni ya kibanda au ni kodi ya ardhi kwa sababu Wafanyabiashara wamejenga vibanda pia alihoji ni kwanini wananchi wanatozwa kodi ya mita wakati wameshalipia gharama za mita wakati wanaomba kufungiwa maji, Afisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo-Ngara alijibu kwamba wafanyabiashara wanalipia eneo lililojengwa kibanda na hawalipi ushuru wa kibanda kwa sababu Halmashauri ndio wamiliki wa maeneo yaliyojengwa vibanda kwa makubaliano kwamba Halmashauri baada ya ujenzi wa vibanda hivyo itakusanya ushuru kila mwezi.

Aidha Mhandisi wa Maji alijibu kwamba wananchi wanalipia gharama za maji pamoja na mita kutokana na maelekezo wanayopewa kama Idara toka EWURA na suala hilo liko sahihi kisheria

Mjumbe mwingine alihoji bajeti ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali haikuwekwa katika bajeti ya mwaka 2017/18, Afisa Maendeleo ya Jamii alijibu kwamba bajeti ya NGO's haiwezi kuingizwa katika mpango wa bajeti wa Halmashaurin kwa sababu fedha zinazopelekwa katika NGO's hazipitishwi kwanza Halmashauri ndipo zipelekwe kwenye NGO's kwa ajili ya matumizi.

Mwenyekiti alisema kwamba Mkurugenzi Mtendaji ahakikishe wale wanaofanya biashara katika vibanda vilivyoko Ngara Mjini wote wamepatiwa mikataba, aidha alitoa ufafanuzi kuwa bajeti zinazowasilishwa na NGO's zinasaidia Halmashauri kuangalia nini kitafanywa na NGO's ili Halmashauri iweze kuangalia vipaumbele vingine vilivyobaki.

Mjumbe mmoja alishauri Idara ya Ujenzi na Zimamoto kuitwa Idara ya Ujenzi peke yake kwa sababu bajeti iliyowasilishwa hakuna sehemu iliyowekwa kwa ajili ya masuala ya moto kama vile ununuzi wa gari la zimamoto, Mhandisi wa Ujenzi alijibu kwamba Idara ya Ujenzi inaitwa Idara ya Ujenzi na Zimamoto kutokana na miongozo inayotolewa na TAMISEMI, hivyo kwa vipindi vinavyokuja unaweza kusikia Idara ya zimamoto ikapelekwa na kuwa chini ya Polisi(W).

Mjumbe mmoja alisema kwamba Wafanyabishara wengi wa vibanda na meza wanalalamika kuchelewa kwa mikataba na wapo ambao mikataba yao imeisha tangu mwezi Agosti, 2016 hali hiyo inaweza kupelekea kudaiwa deni kubwa ambalo wanaweza kushindwa kulipa, aidha alihoji kwamba kama mwananchi amejenga nyumba yake na ameamua kuweka vibanda je atachajiwa kodi ya eneo/ ushuru wa kibanda au atatakiwa kulipia ushuru upi?, Afisa Mtendaji Mamlaka ya Mji Mdogo alijibu kwamba wananchi ambao wamejenga nyumba zao lakini wakaweka vibanda vya biashara Halmashauri itawajibika kukusanya kodi ya leseni na sio kodi ya eneo kama ambavyo wafanyabiashara wengine waliojenga katika maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri wanavyolipia.

Katibu Tawala(W) alimuomba Mkurugenzi Mtendaji kuandika barua kwa RAS kwa ajili ya kukumbushia nyumba zilizoko chini ya RAS kurudishwa/ kukabidhiwa kwa Halmashauri ili ziweze kuongeza kipato.

#### **MUHT NA 14/2016/2017: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na kuwaomba Waheshimiwa Madiwani kuendelea kusimamia Maslahi ya Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kwa manufaa ya wananchi wa Wilaya ya Ngara na kwa manufaa ya nchi ya Tanzania kwa ujumla. Alisisitiza vipaumbele vilivyowekwa vizingatie maslahi ya wananchi wa Wilaya ya Ngara. Kikao kilifungwa saa 6.48 mchana.



**UMETHIBITISHWA NA:**

.....  
Mh. LT. COL. MICHAEL MNTENJELE  
**MWENYEKITI**

.....  
Bw. AIDAN J. BAHAMA  
**KATIBU**

**Tarehe...../.....2016**